



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI

S.L.P 42  
SINGIDA

**MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA BODI YA ZABUNI YA HALMASHAURI YA  
WILAYA IKUNGI CHA TAREHE 30/10/2021 KILICHOFANYIKA UKUMBI WA  
MIKUTANO WA HALMASHAURI**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:**

1. Richard O. Rwehumbiza – Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira- Mwenyekiti
2. Mkome Salige – Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi – Katibu
3. Eva G. Myula – Mkuu wa Kitengo cha Tehama – Mjumbe
4. Dr. Antony Mwangolombe – Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi – Mjumbe
5. Ngwano J. Ngwano – Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari - Mjumbe

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA:**

1. Margaret Kapolesya – Kwa taarifa

**SEKRETARIETI:**

1. Mariam Msangi – Afisa Manunuzi
2. Bahati Peter - Mwandishi wa vikao
3. Faith Mponzi – Afisa Manunuzi

**AGENDA**

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Kupitisha Manunuzi ya ununuzi wa madirisha ya aluminium ujenzi wa nyumba za Wakuu wa Idara na vitengo na nyumba moja ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Ikungi
4. Kupitisha njia ya manunuzi katika kutekeleza miradi ya Uviko 19
5. Kufunga Kikao

### **MUHT. NA. 36/2021/2022 – KUFUNGUA KIKAO**

Katibu aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao akieleza kuwa kikao hiki ni cha kupitisha manunuzi mbalimbali.. Baada ya kusema hayo alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao. Mwenyekiti alifungua kikao saa 10.10 jioni

### **MUHT.NA. 37/2020/2021 – KUTHIBITISHA AGENDA**

Wajumbe waliridhia agenda zilizowasilishwa ziadiliwe

### **MUHT.NA. 38/2020/2021 – KUPITISHA MANUNUZI YA VIFAA MBALIMBALI**

Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa tarehe 18/10/2021 Kitengo cha Manunuzi walipokea muhtasari wa Kamati ya Ujenzi kwa ajili ya ununuzi wa madirisha ya aluminium baada ya kuridhiwa na Mkurugenzi Mtendaji

Baada ya kupokea maombi haya Kitengo cha Manunuzi kwa kuzingatia sheria na Kanuni walifanya quotations kwa wazabuni mbalimbali waliosajiliwa na GPSA, kwa zile bidhaa ambazo hakuna wazabuni waliosajiliwa na GPSA Kitengo kilifanya quotations kwa wafanya biashara mbalimbali na zile huduma za kutengenezwa na mafundi Kitengo cha Manunuzi walifanya quotations kwa mafundi mbalimbali kama ifuatavyo:

#### **1. UNUNUZI WA MADIRISHA YA ALUMINIUM YENYE UKUBWA TOFAUTI TOFAUTI**

Quotations zilitolewa kwa watengenezaji watatu (Local Fundi) kama ifuatavyo:

1. Amini Sitta Alphonce. Aliwasilisha gharama ya Tshs 26,790,000/=
2. Shirika la viwanda vidogo Singida. Waliwasilisha gharama ya Tshs 34,490,000/=
3. Fekason Trading Agency Limited. Aliwasilisha gharama ya Tshs 28,600,000/=

Kitengo cha Manunuzi baada ya kupitia gharama za waombaji walipendekeza kazi hii apewe Amini Sitta Alphonce kwa gharama ya Tshs 26,790,000/=

### **MUHT.NA. 39/2020/2021 – KUPITISHA MANUNUZI YA VIFAA MBALIMBALI**

Katibu aliwasilisha mapokezi ya fedha kiasi cha Tshs 2,730,000,000 ambazo hazikuwa kwenye bajeti na Mpango wa Manunuzi wa Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Aidha Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa fedha hizi zimeletwa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye shule za sekondari, ujenzi wa shule shikizi na ujenzi wa nyumba ya mganga (3 kwa 1) katika Mchanganuo ufuatao:


1. Ujenzi wa nyumba ya mtumishi Tshs 90,000,000.00
2. Ujenzi wa vyumba vya madarasa shule za sekondari Tshs 1,340,000.00
3. Ujenzi wa shule shikizi Tshs 1,3000,000.00

Wajumbe walijadili suala hili na kukubaliana kwamba kwa vile fedha zimepelekwa kwenye akaunti za shule mbalimbali utumike utaratibu wa Force Account ili kuwezesha Kamati za shule kutekeleza kazi hizi kwa muda mfupi na kwa usimamizi wa Karibu.

#### MUHT. NA. 40/2020/2021 – KUFUNGA KIKAO

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afunge kikao. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa ushiriki wao katika kuchangia michango yao ya mawazo. Baada ya kusema hayo alifunga kikao saa 12.30 jioni.

UMETHIBITISHWA

  
.....  
KATIBU

  
.....  
MWENYEKITI

TAREHE 21/01/2022.....

TAREHE 21/01/2022.....